(2) Msajili anaweza, katika muda wowote, kufuta kibali kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) pale ambapo masharti yaliyoainishwa katika leseni hiyo yamekiukwa.

(3) Msajili atawasilisha taarifa ya kila mwaka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi ikijumuisha taarifa kuhusiana na vibali vyote vilivyo tolewa chini ya kifungu hiki, kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(4) Mtu ambaye kwake kibali kimetolewa chini ya kifungu hiki aitatoa au atatumia silaha hiyo kwa kwa kuzingatia masharti yatakayowekwa na Msajili.

Alama ya
utambuzi ya
mtengenezaji

18. Leseni ya silaha haitatolewa kwa mtu yeyote isipokuwa kama silaha hiyo ina namba ya utambulisho ya mtengenezaji au alama nyingine yoyote ambayo kupitia kwake silaha hiyo inaweza kutambuliwa.

Alama ya
utambuzi wa
kitaifa

19.-(1) Silaha zote ndogo na silaha nyepesi zitawekwa alama ya utambuzi wa kitaifa, itakayo amuliwa na Kamati.

(2) Msajili atachonga alama ya utambulisho wa kitaifa katika silaha.

(3) Mmiliki wa silaha ambayo ilikuwa na leseni kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ataiwasilisha kwa Msajili kwa ajili ya kuwekwa alama.

(4) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), Msajili atatoa maelekezo yatakayoelezea muda ambao ndani yake mmiliki atawasilisha silaha yake kwa ajili ya kuwekwa alama na anaweza kutoa adhabu kwa ajili ya kushindwa kutekeleza matakwa ya maelekezo hayo.

(5) Mtu yeyote hatafuta, kurekebisha au kwa namna yeyote ile kubadilisha namba ya utambuzi ya mtengenezaji au alama yeyote ya utambuzi kwa lengo la kubadilisha utambulisho wake.

(6) Mmiliki wa silaha atatoa taarifa mara moja kwa Msajili kuhusiana na silaha yeyote ambayo imefutwa, imerekebisha au kubadilishwa kwa namna yeyote ambayo itaifanya kutokusomeka.

(7) Msajili anaweza, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (6), kuelekeza kimaandishi kwamba silaha iwekwe alama kwa mujibu wa kifungu hiki.

(8) Mtu ambaye anakiuka vifungu vidogo vya (4) na (5) anatenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, atalipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kutumikia kifungu kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Umiliki wa
silaha
kinyume na
sheria

20.-(1) Mtu hatamiliki silaha au sehemu yoyote ya silaha isipokuwa kama-

- (a) anamiliki leseni ya muuzaji, mtengenezaji au leseni ya mfua bunduki au kibali cha muingizaji ndani ya nchi, msafirishaji nje ya nchi, msafirishaji ndani ya nchi au kibali chamsafirishaji kilichotolewa chini ya Sheria hii;
- (b) amedhinishwa kufanya hivyo chini ya sheria nyingine yoyote.

(2) Mtu anayekiuka kifungu hiki anatenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kutumikia kifungo kwa kipindi cha miaka mitano.

(3) Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar na kwa taarifa itakayo chapishwa katika *Gazetila Serikali*, kukataza au kuzuia utwaaji, uuzaji, umiliki au matumizi ya silaha au sehemu ya silaha iwapo-

- (a) ni kwa manufaa ya usalama wa umma; au
- (b) inahitajika kufanya hivyo kwa ajili ya kudumisha amani na utulivu.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, neno “sehemu ya silaha” maana yake ni kikokotoo cha silaha, bolti au kitako cha bunduki.

(c) *Leseni au Kibali cha Kumiliki Risasi*

Umiliki wa
risasi kinyume
na sheria

21. Mtu hatamiliki risasi isipokuwa kama-

- (c) ana leseni halali ya ununuzi, uuzaji, ufuaji bunduki au ya uingizaji ndani ya nchi au usafirishaji nje ya nchi usafirishaji au msafirishaji; au
- (d) vinginevyo amedhinishwa kufanya hivyo chini ya sheria nyingine yoyote.

Kibali **cha**
dadi ya risasi
ambazo mntu
anaweza
kumiliki

22.-(1) Mtu aliye na leseni au kumili silaha hataruhusiwa kumiliki risasi zaidi ya kiwango alichoruhusiwa kumiliki katika leseni yake.

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi 2015 71

(2) Ukomo uliotolewa na kifungu kidogo cha (1) hautatumika kwa mmiliki wa leseni aliyeidhinishwa kumiliki risasi zilizounuliwa na kufyatuliwa katika eneo la ulengaji shabaha lililoidhinishwa.

Katazo la matumizi ya aina fulani za risasi

23. Waziri, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar na kwa tangazo litakalochapishwa katika *Gazeti la Serikali*, kukataza au kuzuia utwaaji, uzaji, umiliki au matumizi ya aina za risasi zilizoainishwa iwapo ni-

- (a) ni kwa manufaa ya umma; au
- (b) inahitajika kwa ajili ya kudumisha amani na utulivu.

Kibali cha kumiliki risasi katika makumbusho binafsi

24.-(1) Msajili ataidhinisha idadi ya risasi zitakazohifadhiwa na taasisi iliyoaidhinishwa.

(2) Risasi zilizokusanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) zinaweza kuhifadhiwa katika makumbusho ya umma.

(3) Msajili anaweza kutoa kibali cha kumiliki silaha katika makumbusho binafsi katika namna itakayoainishwa katika kanuni.

(4) Mhifadhi binafsi hatamiliki zaidi ya risasi 200 katika kipenyo chochote isipokuwa kama Msajili ataidhinisha kiwango cha juu kwa maandishi.

(5) Mmiliki wa kibali kilichotolewa kwa mujibu wa kifungu hiki-

- (c) atahifadhi risasi katika eneo lililoelezwa katika kibali; na
- (d) anaweza kuweka risasi wazi kwa maonyesho kwa mujibu wa taratibu na masharti ya usalama kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Kibali cha kumiliki silaha na risasi cha mkusanyaji wa umma

25.-(1) Msajili anaweza, baada ya kushauriana na Mkurugenzi wa Malikale, kutoa leseni au kibali kwa mhifadhi wa umma kumiliki silaha na risasi kwa ajili ya makumbusho ya umma.

(2) Mmiliki wa kibali kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) hatamiliki zaidi ya risasi 200 katika kipenyo chochote isipokuwa kama Msajili anaidhinisha kiwango kikubwa zaidi kimaandishi.

(3) Silaha na risasi ambazo kwazo kibali kimetolewa chini ya kifungu hiki, zitawekwa wazi kwa maonyesho-

- (e) katika makumbusho yaliyoidhinishwa; na
- (f) kwa mujibu wa masharti kama itakavyoelekezwa katika kanuni.

(4) Mmiliki wa kibali ya matumizi salama kilichotolewa chini ya kifungu hiki hatafyatua risasi yoyote iliyo katika ya hifadhi yake.

(c) Watu Wasio stahili Kumiliki Silaha

Watuwasio na sifa ya kumiliki silaha

26.-(1) Msajili anaweza baada ya kufanya uchunguzi, kumtangaza mtu, ambaye ni mwombaji wa leseni au kibali cha kumiliki silaha au risasi au mmiliki wa leseni au kibali, kuwa hana sifa ya kuomba kibali cha kumiliki silaha iwapo-

- (a) hali ya akili ya mtu huyo, tabia yake ya ukorofi au iwapo ni tegemezi wa ulevi wowote au narkotiki;
- (b) mtu huyo ni hatari kwake yeye mwenyewe au watu wengine;
- (c) mtu huyo ameshindwa kuchukua hatua stahili za kuhifadhi silaha katika sehemu ya usalama;
- (d) mtu huyo ametoa taarifa za uongo au zenye kupotosha kuhusu silaha hiyo kinyume cha Sheria hii; na
- (e) mtu huyo ametiwa hatiani kwa makosa yoyote kati ya yaliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria hii.

(2) Endapo uchunguzi chini ya kifungu kidogo cha (1) umekamilika na Msajili ameridhika kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kuwa mtu hana sifa za kumiliki silaha-

- (a) atatoa notisi kimaandishi itakayowasilishwa kwa mtu huyo akimtaka kufika mbele yake katika muda na sehemu iliyotajwa katika notisi hiyo ilikuonyesha ni kwasababu gani asitangazwe kuwa hana sifa ya kumiliki silaha; na
- (b) pale ambapo mtu ambaye kwaye notisi imetolewa katika kifungu kidogo cha (2)(a) anashindwa kuhudhuria bila sababu za msingi, katika muda na sehemu iliyotajwa katika notisi, atamtangaza kuwa hana sifa za kumiliki silaha.

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi 2015 73

(3) Cheti cha kuonyesha uwezo, leseni na kibali, kilichotolewa kwa mtu yeyote ambaye ametangazwa kuwa hana sifa ya kumiliki silaha chini ya kifungu hiki, vitapoteza uhalali wake kuanzia tarehe ya kutangazwa huko.

(4) Mtu aliyetangazwa kuwa hana sifa kwa mujibu wa kifungu hiki atasalimisha katika kituo cha Polisi kilicho karibu naye, haraka iwezekanavyo-

(a) cheti cha kuonyesha uwezo, leseni na vibali vilivyotolewa kwake; na

(b) silaha pamoja na risasi zilizo katika umiliki wake.

(5) Endapo mtu amesalimisha silaha yake au risasi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), vitashughulikiwa ndani ya muda na kwa namna ambayo itaelekezwa na Msajili katika kanuni.

(d) Hifadhi na Utunzaji wa Silaha na Risasi

Hifadhi na
utunzaji wa
silaha na risasi

27.-(1) Muagizaji ndani ya nchi wa silaha na risasi atalazimika baada ya-

(a) kupata kibali toka kwa afisa muidhiniwa; na

(b) kuzingatia maelekezo yoyote kuhusiana na usafirishaji silaha na risasi;

mara moja atawasilisha silaha na risasi katika maghala ya umma au kituo cha Polisi, kwa ajili ya kuhifadhiwa, kwa gharama zake.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika kwa silaha na risasi zilizoingizwa nchini na au kwa matumizi ya Serikali.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Msajili anaweza, kuhusiana na Tanzania Zanzibar, na kwa kushauriana na Kamishna wa Polisi Zanzibar, kuelekeza sehemu nyingine yoyote ambapo silaha na risasi zitahifadhiwa, na sehemu hiyo inaweza kujumuisha kituo cha polisi.

Muingizaji wa
silaha ndani
ya nchi
kutunza
kumbukumbu

28.-(1) Kila muingizaji wa silaha na risasi ndani ya nchi, haraka iwezekanavyo, baada ya uwasilishaji uliyofanyika chini ya kifungu cha 27, kabla ya kuondoa silaha au risasi yoyote au sehemu yake na kila kifurushi cha risasi ataweka kumbukumbu ya silaha, risasi au sehemu yake yoyote katika namna iliyoelezwa.

(2) Mtu anayeingiza silaha nchini na kuhifadhi silaha na risasi atatoa taarifa hiyo kwa madhumuni ya kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu kufanyika kama itakavyo hitajika na afisa mfawidhi wa ghala, kituo cha polisi au kama itakavyoelezwa na Msajili.

(3) Silaha na risasi zote zilizoingizwa ndani ya nchi kwa madhumuni ya biashara zitasajiliwa katika tarehe amabayo ziliingizwa ndani ya ghala la umma au kituo cha polisi kwa mara ya kwanza.

Utoaji wa silaha na risasi kutoka ghala la umma au kituo cha polisi, nk.

29.-(1) Silaha au risasi zilizohifadhiwa katika ghala la umma, kituo cha polisi au sehemu nyingine yoyote iliyoelezwa na Msajili, hazitatolewa ndani humo isipokuwa kwa kibali kilichosainiwa na Msajili.

(2) Kibali hakitatolewa kwa ajili ya uondoaji wa silaha au risasi isipokuwa kama Msajili ameridhika kwamba ni-

(a) kwa ajili ya kupelekwa katika sehemu zilizotajwa na Waziri, pale ambapo wakazi wanaruhusiwa kubeba au kumiliki silaha chini ya udhibiti na jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa madhumuni ya ulinzi dhidi ya majambazi, wanyamahatari au waasi;

(b) kwa ajili ya kupelekwa katika ghala jingine la umma au, kituo kingine cha Polisi; au

(c) kwa ajili ya watu binafsi ambao wanaweza kuonyesha kuwa wanahitaji silaha na risasi kwa ajili ya matumizi yao halali.

(3) Kibali kitaelezea sehemu na muda ambao ndani yake silaha na risasi zitasafirishwa baada ya kuondolewa na sehemu ambayo zinatakiwa kuhifadhiwa kwa kipindi hicho.

(4) Msajili anaweza kuweka ukomo wa kiasi cha silaha na risasi zitakazoruhusiwa kutolewa katika muda wowote.

(5) Kabla ya kuruhusu uondolewaji wa silaha au risasi, Msajili anaweza kuhitaji ulinzi huo kutolewa kadri ambavyo ataona inafaa ili kuhakikisha kuwa masharti ya Sheria hii yanazingatiwa.

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi 2015 75

(6) Kila kibali cha utoaji wa silaha au risasi kitaanisha alama, nambari na maelezo ya silaha au risasi hiyo.

Mamlaka ya
Inspekta
Jenerali wa
Polisi katika
kuhifadhi
silaha

30.-(1) Bila kuathiri masharti yoyote ya sheria nyingine kuhusiana na namna ya kuhifadhi silaha na risasi, Inspekta Jenerali wa Polisi aweza kutoa maelekezo ya namna ya kuhifadhi silaha na risasi ambazo zinafika mikononi mwa polisi na anaweza kutoza ada kwa utunzaji huo.

(2) Inspekta Jenerali wa Polisi aweza kupeleka maombi kwa Hakimu Mkazi kwa ajili ya kuomba amri ya kutaifisha silaha na risasi iwapo zimehifadhiwa kwa kipindi hadi kufikia miezi kumi na nane au pale ambapo ada chini ya kifungu kidogo cha (1) haijalipwa ndani ya miezi miwili baada ya tarehe ya utunzaji.

(3) Endapo kuhusiana na maombi chini ya kifungu cha (2) Hakimu Mkazi anaridhika kwamba-

(a) hatua stahiki zimechukuliwa ili kuyafikisha maombi kwa ufahamu wa mtu ambaye anaelekea kuwa ndiye mmiliki wa silaha au risasi;

(b) mtu huyo amepewa fursa stahiki ya kulipa ada au kuchukua hatua za kisheria za kuhifadhi silaha au risasi, na anashindwa kufanya hivyo,

Hakimu Mkazi ataamuru silaha au risasi hizo kutaifishwa kwa Serikali.

Masharti
kuhusiana na
Tanzania
Zanzibar

31.-(1) Bila kujali kifungu cha 8, Kamishna wa Polisi wa Tanzania Zanzibar atakuwa Msajili kwa Tanzania Zanzibar.

(2) Leseni ya kumiliki silaha iliyotolewa Tanzania Bara haitatokuwa halali kwa madhumuni sawa kuhusiana na silaha hiyo au silaha nyingine na risasi ndani ya Tanzania Zanzibar isipokuwa kama imesainiwa na Msajili au afisa muidhiniwa.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) yatatumika pamoja na marekebisho stahiki, kwa upande wa Tanzania Bara.

(4) Mtu anaweza kubeba, kumiliki au kutumia silaha au risasi yoyote ndani ya Tanzania Zanzibar, isipokuwa atatunza au kuhifadhi silaha na risasi kwa mujibu wa maelekezo ya Msajili, baada ya matumizi hayo.

SEHEMU YA NNE

LESENI NA VIBALI VYA WAUZAJI, WATENGENEZAJI NA WAFUA BUNDUKI

(c) *Wauzaji wa Silaha*

Kibali cha muuzaji wa silaha

32.-(1) Msajili hatatoa kibali cha shughuli yoyote ile ya silaha, mbali na silaha zisizojifyatua zenyewe (non-automatic) isiokuwa kama ameshauriana na kupata ridhaa ya Bodi ya Ushauri ya Udhibiti wa Silaha.

(2) Mtu anayekusudia kujishughulisha na biashara ya silaha au risasi-

Sura ya 212

(a) atakuwa na leseni ya muuzaji;

(b) iwapo muombaji ni kampuni, itasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni.

(3) Maombi yoyote ya kibali cha kufanya biashara ya silaha au risasi yatafanywa kwa Msajili katika fomu maalum kama ilivyoainishwa katika kanuni.

Masharti yaliyoweka kwa muuzaji

33. Waziri, baada ya kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, anaweza kutunga kanuni zitakazoelezea-

(a) masharti kuhusiana na utoaji wa kibali cha muuzaji;

(b) masharti ambayo Msajili ataweka kwa wauzaji;

(c) maelezo kuhusiana na eneo la biashara la muuzaji;

(d) utaratibu wa kutolewa upya kwa kibali cha muuzaji; na

(e) kusitishwa na kufutwa kwa muda kwa kibali cha muuzaji.

Kubadili maeneo

34.-(1) Muuzaji ataendesha biashara ya silaha na risasi katika eneo lililotajwa katika kibali cha muuzaji.

(2) Endapo muuzaji anakusudia kubadili eneo la biashara, atawasilisha maombi ya kibali kwa madhumuni hayo.

(3) Maombi ya kubadilisha eneo la biashara yatawasilishwa kwa Msajili katika namna itakayoelezewa kwenye kanuni.

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi 2015 77

(4) Endapo Msajili anaridhika na maombi kwa ajili ya kubadili eneo, anaweza kuidhinisha leseni iliyopo au kutoa leseni mpya itakayoainisha masharti ambayo anaona ni muhimu kuyaweka kwa ajili ya mabadiliko.

Wajibu wa muuzaji

35.-(1) Muuzaji atatumza rejesta katika eneo lake la biashara, kama itakavyoelezewa katika kanuni, itakayokuwa na taarifa zilizoainishwa katika kibali cha muuzaji.

(2) Muuzaji atahakikisha kuwa kibali cha muuzaji muda wote kinawekwa katika sehemu ya wazi iliyo ndani ya eneo lake la biashara.

(3) Muuzaji, pale atakapo kuhitajika kufanya hivyo na Msajili, ataweka wazi kwa ukaguzi-

(a) silaha au risasi yoyote ambao muuzaji anao kwenye hifadhi yake;

(b) kibali chake cha muuzaji; na

(c) kumbukumbu nyingine zozote ambazo afisa muidhiniwa anaweza kuzihitaji kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi chini ya Sheria hii.

(4) Muuzaji aliyeidhinishwa atawasilisha kwa Msajili marejesho ya biashara alizoendesha ndani ya kipindi kilichoainishwa katika fomu iliyoainishwa.

Namna ya kuhifadhi silaha baada ya kusitishwa kwa biashara

36. Endapo mtu anayemiliki leseni iliyotolewa kwa mujibu wa Sehemu ya Tatu anaacha kuendesha biashara kwa sababu yoyote ile, atatumza silaha na risasi zilizo katika sehemu itakayotajwa na Msajili.

Matumizi ya sheria nyingine

37. Kibali kilichotolewa chini ya Sehemu hii hakitatoa msamaha kwa mmiliki wa kibali kutekeleza masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusiana na utoaji leseni za biashara.

(d) Watengenezaji, Wafua Bunduki na Mawakala

Katzo la kutengeneza silaha au risasi

38.-(1) Mtu hataruhusiwa kutengeneza, kuunganisha silaha au risasi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya kibali kilichotolewa na Bodi ya Udhhibiti na Ushauri wa Silaha.

78 2015 Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi No.2

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Bodi inaweza kuruhusu kitolewe kibali cha kutengeneza silaha, kwa kuzingatia kwamba mwombaji atakuwa ametimiza vigezo na masharti.

Ukarabati wa silaha

39.-(1) Mtu hataruhusiwa kukarabati silaha isipokuwa kama anamiliki kibali cha ufuaji wa bunduki chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), mtu -

(c) hatabadilisha muundo wa silaha ili kuiwezesha kufyatua zaidi ya risasi moja pale ambapo bunduki hiyo inafyatuliwa mara moja; na

(d) badilisha kikokotoo cha silaha au urefu wa mtutu wa silaha hiyo;

(3) Silaha zote zitafanyiwa ukarabati katika karakana ya Serikali au na mfua bundkialiyeye na leseni.

Idhini ya Bodi ya Udhibiti na Ushauri wa Silaha

40. Bila kujali masharti yoyote ya Sheria hii, Msajili hatatoa kibali cha mfua bunduki isipokuwa kama mwombaji ameidhinishwa na Bodi ya Udhibiti na Ushauri wa Silaha.

Masharti ya leseni ya mfua bunduki

41. Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa Tanzania Zanzibar, kuelezea-

(a) namna ya utolewaji, usitishaji wa muda, ufutaji na utolewaji upya wa kibali cha ufuaji wa bunduki;

(b) masharti ambayo Msajili anaweza kuambatanisha katika kibali cha ufuaji bunduki; na

(c) maelezo kuhusiana na eneo la biashara la ufuaji bunduki.

Kibali cha uwakala

42. Mtu hatafanya majadiliano au kupanga mikataba, manunuzi, uuzaji au ubadilishaji wa silaha na risasi kwa niaba ya mtu mwingine kwa ajili ya malipo, kamisheni au faida nyingine yoyote isipokuwa kama mtu huyo anamiliki leseni ya muuzaji iliyotolewa chini ya Sheria hii.

Utolewaji wa kibali cha uwakala

43. Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kuelekeza-

(a) utaratibu wa utolewaji, usimamishaji wa leseni kwa muda au utolewaji upya wa kibali cha ufuaji wa bunduki;

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi 2015 79

- (b) masharti ambayo kwayo Msajili anaweza kuambatanisha katika kibali cha uwakala; na
- (c) maelezo kuhusiana na eneo la biashara la wakala.

Idhini ya Bodi
ya Udhhibiti na
Ushauri wa
Silaha

44. Bila kujali masharti yoyote ya Sheria hii, kibali cha uwakala hakitatolewa kwa ajili ya uendeshaji wa biashara ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa kama muuzaji ameidhishwa na Bodi ya Udhhibiti na Ushauri wa Silaha.

SEHEMU YA TANO

**UINGIZAJI NDANI YA NCHI, UPITISHAJI NDANI YA NCHI NA
USAFIRISHAJI WA SILAHA NA RISASI**

(a) Uingizaji Ndani ya Nchi, Usafirishaji Nje ya Nchi na Upitishaji Ndani ya Nchi wa Silaha na Risasi

Uingizaji ndani
ya nchi,
usafirishaji nje
a nchi na
upitishaji ndani
ya nchi

45.-(1) Mtu hataruhusiwa kuingiza ndani ya nchi, kusafirisha nje ya nchi au kusafirisha ndani ya nchi silaha au risasi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kibali.

(2) Mtu hataruhusiwa kuingiza ndani ya nchi silaha au risasi isipokuwa-

- (a) Kama ni kwa matumizi binafsi;
- (b) kama ana hati ya mtumiaji wa mwisho kutoka kwa Msajili; na
- (c) ni muuzaji aliyeidhinishwa chini ya Sheria hii.

(3) Mtu anayeingiza ndani ya nchi au anayesafirisha nje ya nchi au anapitisha silaha au risasi ndani ya Jamhuri ya Muungano, iwapo ni kwa biashara au kwa matumizi binafsi, ataomba leseni tofauti kwa kila mzigo ambao unaingizwa ndani ya nchi au kusafirishwa nje ya nchi.

(4) Silaha au risasi zinazolingizwa ndani ya nchi zitashushwa katika maeneo ya kuingilia nchini kama ylivyotajwa katika Sheria ya Ushuru wa Forodha.

Sura ya 403

80 **2015** *Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi No.2*

Leseni ya
upitishaji silaha
ndani ya nchi
kwenda nchi
jirani

46. Bila kujali jambo lolote ndani ya Sheria hii, kibali cha upitishaji wa silaha au risasi ndani ya nchi, iwapo ni silaha au risasi kamili au sehemu yake kwenda nchi jirani, kinaweza kutolewa, kusitishwa kwa muda, kukataliwa, kutoewa upya au kufutwa na Waziri kwa mujibu wa masharti ya ibara ya kumi ya Mkataba unaorejewa katika Jedwali la Nne.

Masharti ya
kibali

47.-(1) Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kutunga kanuni zitakazoelezea-

- (a) namna ya utolewaji, usitishwaji kwa muda, ufutwaji au utolewaji upya wa vibali vya uingizaji ndani ya nchi, usafirishaji nje ya nchi au upitishaji ndani ya nchi;
- (b) masharti ambayo Msajili ataweka kwa mmiliki wa kibali;
- (c) sifa za muombaji wa kibali cha umiliki; na
- (d) alama za utambuzi.

Ukaguzi

48.-(1) Mmiliki wa kibali kitakachotolewa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, iwapo atahitajika kufanya hivyo na Msajili, ataweka wazi kwa ukaguzi-

- (d) silaha au risasi zozote zilizo katika umiliki au zilizo katika uangalizi wake;
- (e) kibali chake; na
- (f) kumbukumbu zozote zinazoweza kutunzwa na yeye kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Muuzaji ataweka na kutunza kumbukumbu za uingizaji ndani ya nchi au uuzaji wa silaha au risasi katika namna itakavyoelekezwa na Msajili.

(b) Usafirishaji wa Silaha na Risasi

Kibali cha
msafirishaji

49.-(1) Mtu hatasafirisha silaha au risasi zozote isipokuwa kama anakibali cha msafirishaji.

(2) Maombi ya kibali cha msafirishaji yatafanywa kwa Msajili katika fomu itakayoainishwa katika kanuni.

Masharti ya
usafirishaji wa
silaha

50. Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar , kuelezea-

- (d) namna ya utoaji, usitishaji, ufutaji au utolewaji upya wa kibali cha msafirishaji;
- (e) masharti ya kibali; na
- (f) sifa za mmiliki wa kibali.

Wajibu wa
msafirishaji

51.-(1) Mmiliki wa kibali cha msafirishaji, pale atakapohitajika kufanya hivyo, ataweka wazi kwa ukaguzi-

- (e) silaha au risasi zozote anazomiliki au zilizo chini ya uangalizi wake;
- (f) kibali chake;
- (g) rejesta au kumbukumbu ambazo zinaweza kutunzwa na yeye; na
- (h) taarifa nyingine yoyote ambayo inaweza kuwa muhimu kwa ukaguzi huo.

(2) Msafirishaji atatumiza na kuweka kumbukumbu za silaha au risasi zote zilizosafirishwa katika namna itakayoelezewa na Msajili na atatoa taarifa zinazohitajika kwa afisa muidhiniwa.

Matumizi ya
Sheria
nyingine

52. Kibali kilichotolewa chini ya Sehemu hii hakittoa msamaha kwa mtu, ambaye kwake kibali hicho kimetolewa, kutotekeleza masharti ya sheria nyingine yoyote ya Bunge kuhusiana na utoaji lesseni za biashara.

SEHEMU YA SITA UPEKUZI NA UKAMATAJI

Upekuzi na
ukamataji

53.-(1) Bila kujali masharti ya sheria yoyote kinyume na hayo, afisa muidhiniwa ambaye ana sababu za msingi za kuwa na mashaka kuwa silaha au risasi inahifadhiwa kinyume na sheria, anaweza katika muda wowote, wakati akiwa anatekeleza majukumu yake-

- (c) kumsimamisha na kumpekua mtu yeyote, gari, chombo cha majini au ndegewakati wa kuingia au kutoka;
- (d) kuingia, na kukamata silaha yoyote au risasi katika eneo lolote.

(2) Endapo afisa muidhiniwa akiwa anatekeleza masharti ya hati ya upekuzi ana kuwa na sababu za msingi kuamini kuwa mtu silaha au risasi yoyote iliyokutwa katika eneo lolote, meli au chombo zinahifadhiwa, kusafirishwa, kushushwa au kuuzwa kinyume na Sheria hii, anaweza kukamata silaha au risasi hizo hadi kipindi ambacho mahakama itakapoamua iwapo silaha au risasi hizo zitaifishwe au la.

Sura ya 20

(3) Masharti ya Sehemu ya Pili ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai kuhusiana na upekuzi na ukamataji yatatumika pamoja ma marekebisho stahiki, kwa Sheria hii.

Kinga kwa mtu anayezuia silaha

54. Hakuna mashitaka au hatua zozote za kisheria zitakazochukuliwa dhidi ya Msajili au afisa yeyote muidhiniwa anayetekeleza mamlaka yoyote au majukumu yoyote chini ya Sheria hii, kwa lolote atakalolitenda kwa nia njema.

SEHEMU YA SABA

KUHIFADHI SILAHA AU RISASI

Utunzaji wa silaha pale kifo kinatokea

55. Endapo mmiliki wa silaha anafariki wakati bado anamiliki silaha, silaha hiyo itahifadhiwa katika namna itakayoelezewa katika kanuni.

Utaifishaji wa silaha zinazohusiana na kosa

56. Silaha au risasi yoyote au ambayo inahusika na kosa, iwapo mahakama itaona inafaa, itataifishwa kwa Serikali.

Utaifishaji wa silaha au risasi zisizo kuwa na mmiliki

57.-(1) Silaha au risasi yoyote iliyopatikana katika jengo lolote, chombo, ndege au sehemu yoyote bila ya kuwa na muelekeo wa kumilikiwa na mtu, inaweza kutaifishwa kwa Serikali.

(2) Endapo silaha au risasi imetaifishwa kwa Serikali kwa amri ya mahakama, itaharibiwa katika namna na ndani ya muda uliotajwa katika amri hiyo ya mahakama.

(3) Amri ya kuharibu silaha hiyo hautatekelezwa na Serikali iwapo kuna rufaa ambayo haijaamuliwa dhidi ya amri hiyo au hadi hapo muda uliotolewa kisheria wa kukata rufaa unapita bila ya rufaa yoyote kufunguliwa dhidi ya amri hiyo.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI MENGINEYO

Ofisi za
Masijala
Kuu ya
Silaha

58.-(1) Masijala kuu ya silaha itakuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dar es Salaam na ofisi ndogo Zanzibar katika eneo ambalo ni sawa na Makao Makuu ya Polisi Tanzania Bara.

(2) Masijala Kuu ya Silaha itakuwa chini ya usimamizi wa Inspekta Jenerali wa Polisi au afisa mwingine kama ambavyo Waziri atakavyomteua, kwa ajili ya kuingiza taarifa za vibali na leseni zote zilizotolewa chini ya Sheria hii.

(3) Msajili atawasilisha kwa Masijala Kuu ya Silaha, kila mwanzoni mwa mwezi, kumbukumbu ya vibali na leseni alizozitoa mwezi uliopita.

Utunzaji
salama wa
silaha na
risasi

59.-(1) Mtu anayemiliki, anayedhibiti au anayetunza silaha au risasi zozote -

(a) atachukua tahadhari ili kuzuia silaha au risasi kutoingia katika mikono, uangalizi au umiliki wa mtu asiyeidhinishwa;

(b) atatekeleza hatua za kiusalama, kwa kuzingatia masharti ya utunzaji salama wa silaha au risasi, na masharti ambayo chini yake silaha au risasi itahifadhiwa, kama ambavyo Msajili atakavyoelekeza.

(2) Katika mwenendo wowote chini ya kifungu hiki au kanuni kuhusu wajibu wa kuchukua hatua za kiusalama, jukumu la kuthibitisha vinginginevyo litakuwa kwa mtu aliyeshitakiwa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki “asifa muidhiniwa” maana yake ni mtu ambaye hajaidhinishwa kumiliki silaha au risasi chini ya Sheria hii.

Makosa na
adhabu

60.-(1) Mtu atakaye kiuka masharti ya Sheria hii, anatenda kosa na atawajibika, atakapotiwa hatiani, isipokuwa pale ambapo adhabu imetolea na sheria nyingine kwa kosa kama hilo, kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano au vyote.

84 **2015 Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi No.2**

(2) Endapo mtu ambaye ametiwa hatianai chini ya kifungu kidogo cha (1) anamiliki kibali cha miliki silaha au risasi, kibali hicho kitafutwa au kusitishwa kwa muda na silaha au risasi zitataifishwa kwa kipindi ambacho mahakama itaona inafaa.

Uhifadhi wa silaha au risasi

61. Mtu atakayeshindwa kuhifadhi salama silaha au risasi ambayo anamiliki kihalali, atakuwa anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni mbili au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au vyote.

Utoaji wa taarifa ya upotevu wa silaha

62.-(1) Endapo silaha au risasi inamilikiwa kihalali na mtu yeyote inapotea, kuibiwa au kuharibika, mtu huyo atatoa taarifa ya upotevu, wizi au uharibifu huo wa silaha au risasi ndani, si zaidi ya siku saba za kazi baada ya kugundua upotevu, wizi au uharibifu huo yeye mwenywe au kupitia kwa mtu aliyeidhinishwa naye kwa kimaandishi, akitoa maelezo kamili ya silaha hiyo au risasi, muda, mahali na mazingira ambayo silaha hiyo au risasi ilipotea, iliibiwa au iliharibika kama afisa mhusika atakavyoelekeza.

(2) Mtu anayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) anatenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote.

Dhana

63.- Kwa kuzingatia kifungu cha 62, pale ambapo imethibitishwa kuwa mshitakiwa katika muda fulani alikuwa kisheria ni mmiliki wa au anamiliki leseni au ameruhusiwa kumiliki silaha au risasi inayoshukiwa kupotea, kuibiwa au kuharibiwa, itakwa ni ushahidi tosha-

- (a) kuwa silaha au risasi hizo zimepotea, kuibiwa au kuharibiwa, kama itathibitika kuwa ameshindwa kuonyesha silaha au risasi atakapo takiwa kufanya hivyo na kanuni yoyote, anshindwa kutoa sababu za msingi za kushindwa huko ;
- (b) ameshindwa kutoa taarifa ya wizi, upotevu au kuharibika kwa silaha kama anavyotakiwa.

Msamaha
kwa
usalimishaji
wa silaha

64.-(1) Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, na kwa Tangazo litakalo chapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*-

(a) kwa madhumuni ya kusalimisha silaha zinazomilikiwa kinyume na sheria; na

(b) kudumisha amani na utulivu,

kutangaza msamaha kwa mtu yeyote atakayepatikana akiwa anamiliki silaha au risasi kinyume na sheria.

(2) Taarifa ya kifungu kidogo cha (1) itabainisha mtu anayepewa msamaha, muda, eneo na masharti ya msamaha huo.

(3) Mtu atakayesalimisha silaha au risasi chini ya kifungu hiki hatashitakiwa.

Maeneo
ambayo
silaha
haziruhusiwi

65.-(1) Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kutangaza eneo lolote, majengo au makundi ya majengo kuwa ni sehemu ambazo silaha haziruhusiwi.

(2) Afisa muidhiniwa anaweza, iwapo ana sababu za kuamini kwamba silaha yoyote imetunzwa kwenye eneo ambalo silaha haziruhusiwi-

(a) kupekua jengo au eneo lolote;

(b) kumpekua mtu yeyote aliyeko kwenye eneo ambalo silaha haziruhusiwi;

(c) kukamata silaha au risasi iliyokutwa kwenye eneo ambalo silaha haziruhusiwi; au

(d) kumtia mbaroni mtu yeyote anayekiuka tangazo lililotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1).

Uhakiki wa
kumbukumbu
u za silaha
au risasi

66. Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar; na iwapo ni kwa maslahi ya umma kufanya hivyo, kumtaka mmiliki yeyote au wamiliki wote wa leseni kuhakiki kumbukumbu zao za silaha au risasi.

Oparesheni
za pamoja

67. Kwa madhumuni ya kudhibiti uzagaaji haramu wa silaha na risasi, Inspekta Jenerali wa Polisi anaweza, kwa mashauriano na Waziri, kumwidhinisha mtu yeyote kushiriki kwenye operesheni zozote za pamoja za kikanda.

Kupeana
taarifa na
kushirikiana

68. Inspekta Jenerali wa Polisi anaweza, kwa madhumuni ya kudhibiti uzagaaji haramu wa silaha na risasi-

- (a) baada ya maombi kutoka kwa mamlaka husika ya nchi nyingine, kutoa kwa mamlaka hiyo taarifa yoyote aliyo nayo; na
- (b) kupokea na kuifanyia kazi taarifa yoyote iliyopatikana kutokana na upelelezi unaouhisiana na silaha au risasi inayomilikiwa isivyo halali.

Makundi ya
silaha zisizo
hatari

69.-(1) Silaha zifuatazo hazitachukuliwa kuwa ni silaha hatari-

- (a) kifaa au silaha iliyotengenezwa kwa matumizi kwenye machinjio kwa ajili ya kuchinjia wanyama;
- (b) silaha ya kutuliza isiyo ya moto;
- (c) silaha ya kuwekea alama;
- (d) silaha ya ishara;
- (e) fataki;
- (f) silaha inayotumika;na
- (g) zinazokataza au zinazodhibiti umiliki, uuzaji, ununuzi na uhamishaji wa baruti na vifuniko vyake unaofanywa na au kutoka kwa mamlaka
- (h) kifaa kingine chochote ambacho Waziri anaweza kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar kwa tangazo la Serikali kwenye Gazeti, kusamehe.

Silaha
bandia

Sura ya 16

70.-(1) Silaha yoyote bandia, bila kujali kwamba haina risasi au kwa namna yeyote ile haiwezi kufyatua risasi, au kutoa kombora, itachukuliwa kwamba ni silaha au kifaa cha hatari kwa madhumuni ya kifungu cha 286 cha Kanuni za Adhabu.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno “silaha bandia au silaha ya kuchezea” maana yake ni kitu chochote chenye muonekano wa silaha ya aina yoyote.

(3) Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanaania Zanzibar, kutengeneza kanuni zitakazoweka utaratibu wa kuingiza nchini silaha bandia au silaha ya kuchezea.

Ada

71. Msajili atatoza ada kwa huduma zinazotolewa chini ya Sheria hii kwa kiwango kitakachoainishwa kwenye kanuni.

Mamlaka ya
kutunga
kanuni

72.-(1) Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kutunga kanuni-

- (a) zinazoainisha-
 - (i) watu ambao watapewa leseni au kibali;
 - (ii) namna ambayo leseni au kibali itakavyokuwa;
 - (iii) vigezo na masharti kuhusu leseni au kibali;
 - (iv) ada itakayotowazwa kwa leseni au kibali; na
 - (v) ufutaji wa leseni yoyote au kibali;
- (b) zinazodhibiti uwekaji muhuri alama namba na usajili wa silaha au risasi;
- (c) utaratibu wa uanzishwaji na usimamiaji wa maghala ya umma na maghala binafsi kwa madhumuni ya Sheria hii;
- (d) usimamiaji na ufuatiliaji wa makampuni binafsi ya ulinzi;
- (e) zinazokatiza au zinazodhibiti umiliki, uuzaji, ununuzi na uhamishaji wa baruti na vifuniko vyake unaofanywa na au kutoka kwa mamlaka ya serikali za mitaa au watu wanaotekeleza majukumu yao kwa niaba ya mamlaka ya serikali za mitaa;
- (f) zitakazoainisha muundo na namna ambayo rejesta yoyote au kumbukumbu zitakazohitajika chini ya Sheria hii zitakavyotunzwa na kukaguliwa;
- (g) zinazozuia na kudhibiti usafirishaji wa silaha na risasi;
- (h) zinazoainisha ada, kodi na gharama za matumizi ya maghala ya umma na namna zitakavyokusanywa;
- (i) zinazoainisha hatua za kiusalama, zinazohusiana na utunzaji salama wa silaha na risasi na mazingira ambayo zitatunzwa au kuchukuliwa na mmiliki wa silaha yoyote au risasi;

- (j) zinazoainisha ada na malipo ya ada zinazopaswa kulipwa kutokana na utolewaji au utolewaji upya wa cheti cha kuthibitisha uwezo, leseni au kibali au kutokana na kitu kingine chochote ambacho kinatakiwa kulipiwa ada inaweza kwa mujibu wa Sheria hii;
- (k) zinazoainisha utunzaji salama wa silaha au risasi zinazomilikiwa na kampuni za ulinzi, taasisi na makampuni mengine binafsi;
- (l) zinazoainisha usalama wa majengo ambayo mawakala, wazalishaji, wafua bunduki, waingizaji nchini na wasafirishaji nje ya nchi wa silaha na risasi, watumiaji wa silaha kwa madhumuni ya biashara ikiwemo tahadhari na taratibu zinazopaswa kuchukuliwa ili kuzuia wizi au matumizi yasiyo halali la silaha na risasi zinazomilikiwa na watu hao;
- (m) zinazoainisha tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa wakati wa kusafirisha, kutumia, kuhifadhi au wakati wa kuteketeza silaha na risasi;
- (n) zinazoainisha namna ya kusalimisha na kufuta vyeti vya uwezo, leseni au vibali vilivyotolewa chini ya Sheria hii, ambavyo vimesitishwa au vimefutwa au ambavyo muda wake kwisha;
- (o) zinazoainisha mafunzo, majaribio na hatua nyingine zozote zitakazoonekana ni muhimu ili kuhakikisha uwezo wa watu ambao wanaweza kumilikishwa na kutumia silaha;
- (p) utaratibu wa kuharibu silaha na risasi chini ya Sheria hii; na
- (q) zinazoainisha suala lingine lolote ambalo Waziri anaona ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi 2015 89

(2) Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii zinaweza kutoa adhabu kwa ukiukwaji wa masharti yoyote yaliyotolewa chini ya Kanuni hizo.

(3) Wakati wa kutekeleza mamlaka yak echini ya kifungu hiki, Waziri anaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika iliyo Tanzania Zanzibar, kutengeneza kanuni mahsusi kwa ajili ya Tanzania Zanzibar.

SEHEMU YA TISA
MAREKEBISHO YATOKANAYO
SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

Tafsiri Sura
ya 260

75. Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, ambapo hapa itarejewa kama “sheria Kuu”.

Marekebisho
ya kifungu
cha 7

76. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 7
kwa-
(c) kufuta kifungu kidogo cha 1(l); na
(d) kuzipanga upya aya za (m) hadi (z) kuwa (l) mpaka
(y).

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7(3))

Shughuli na Masuala Yanayohusiana na Kamati

Muda wa kukaa
madarakani

1.-(1) Kila Mjumbe wa Kamati atakuwepo madarakani kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja .

(2) Waziri anaweza kufanya mabadiliko au kurekebisha orodha ya wajumbe wa Kamati.

(3) Katika kuteua wajumbe wa Kamati, Waziri atazingatia usawa wa kijinsia pamoja na usawa katika uwakilishi kwa wajumbe wanaotoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Uteuzi wa
mjumbe wa
muda

2.-(1) Endapo mjumbe, kwa sababu ya ugonjwa, ulemavu au kutokuwepo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, havezi kuhudhuria kikao chochote cha Kamati bila ya sababu yoyote ya msingi, mamlaka ya uteuzi inaweza kuteua mtu mwingine badala yake na mtu huyo atakoma kuwa madarakani baada mjumbe aliyekuwepo kurudi madarakani.

90 2015 Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi No.2

(2) Endapo mjumbe anashindwa kurudi madarakani ndani ya muda wa miezi sita, Waziri atamthibitisha mjumbe aliyeteuliwa chini ya aya ndogo ya (1) kushika madaraka.

Makamu
Menyekiti

3. Kamati itachagua mmoja wa wajumbe wake kuwa Makamu Mwenyekiti, na mjumbe yeyote atakayechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti, kushika madaraka hayo kwa kipindi cha mwaka mmoja toka tarehe ya kuchaguliwa kwake na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

Mamlaka ya
Mwenyekiti na
Makamu
Mwenyekiti

4.-(1) Mwenyekiti ataendesha vikao vyote vya Kamati.
(2) Endapo katika kikao chochote cha Kamati Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao.
(3) Ikiwa wote wawili, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo katika kikao chochote cha Kamati, wajumbe waliopo wanaweza kuchagua miongoni mwao Mwenyekiti wa muda ambaye ataendesha kikao hicho.

Vikao na
taratibu za
Kamati

5.-(1) Kamati itakutana siyo chini ya mara nne kwa mwaka na wakati mwingine wa ziada unaoweza kuwekwa na Mwenyekiti au kama hatakuwepo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kama hataweza kwa sababu zozote kufanya hivyo, Makamu Mwenyekiti.

(2) Mwenyekiti na, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti wanaweza, baada ya kupokea maombi ya wajumbe angalau watano, kuitisha kikao mahsusi cha Kamati wakati wowote.

(3) Katibu Mtendaji wa Kamati atamtaarifu kila mjumbe katika muda wa kutosha, muda na mahali ambapo kila kikao kitafanyika.

Akidi

6. Katika kikao chochote cha Kamati akidi itakuwa si chini ya nusu ya wajumbe waliopo.

Uamuzi wa
Kamati

7. Masuala yote kwenye kikao chochote cha Kamati yataamuliwa kwa njia ya makubaliano ya pamoja.

Kumbukumbu
za mwenendo
wa Kamati

8.-(1) Kamati itaweka kumbukumbu za shughuli zote za vikao vya Kamati kwenye kitabu maalum kitakachowekwa kwa sababu hiyo.

(2) Muhtasari wowote ulioidhinishwa na kusainiwa na Mwenyekiti wa kikao kinachofuata utakuwa ni ushahidi kwamba kikao husika kiliitishwa kihalali.

Kutohudhuria
vikao vitatu
mfululizo

9. Endapo mjumbe yeyote hajahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Kamati bila ya kuwa na sababu za msingi, Kamati itaijulisha mamlaka ya uteuzi juu ya jambo hilo na mamlaka ya uteuzi inaweza kusitisha uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mjumbe mwingine kuchukua nafasi yake pale itakapona inafaa kufanya hivyo.

Mwenendo wa Kamati **10.** Kamati inaweza kujiwekea utaratibu wa kuendesha vikao vyake.

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 26(e))

MAKOSA YANAYOMWONDOLEA MTU SIFA ZA KUMILIKI SILAHA

1. Makosa chini ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi.
2. Makosa chini ya Sheria ya Kuzuia Matumizi ya Madawa na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya.
3. Makosa chini ya Sheria ya Kanuni za Adhabu.
4. Makosa chini ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu.
5. Makosa chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.
6. Kula njama kwa namna yoyote, uchochezi au kujaribu kutenda kosa lililoainishwa katika Jedwali hili.

JEDWALI LA TATU

(Limetungwa Chini ya Kifungu cha ya kifungu cha 13(2))

NCHI ZENYE MAKUBALIANO YA UTAMBUZI SAWA

- (a) Kenya;
- (b) Uganda;
- (c) Rwanda;
- (d) Burundi;
- (e) Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;
- (f) Jamhuri ya Kongo;
- (g) Zambia;
- (h) Malawi;
- (i) Zimbabwe; au
- (j) Msumbiji.

JEDWALI LA NNE

(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 46)

Itifaki ya Kimataifa juu ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha au vipuri vyake pamoja na Risasi, Nyongeza ya Azimio la Kimataifa Dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa, G.A. Azimio Na. 255, la Novemba. 15, 2000, U.N. Doc. A/RES/55/255 (2001), *haijaanza kutumika.*

Ibara ya Kumi

Masharti ya jumla kuhusiana na usafirishaji nje ya nchi, uingizaji ndani ya nchi na usafirishaji kupitia nchini au mifumo ya uidhinishaji.

1. Kila Nchi Mwanachama itaanzisha na kutunza mfumo mahsusi ya leseni za usafirishaji nje ya nchi, uingizaji ndani ya nchi na uidhinishaji, pamoja na masharti kuhusiana na upitishaji wa silaha nchini kwenda mataifa mengine kwa lengo la uhamishaji wa silaha au vipuri vyake pamoja na risasi.

2. Kabla ya kutolewa kwa leseni au uidhinishaji usafirishaji silaha, risasi na vipuri vyake, kila nchi mwanachama itahakikisha:

- (a) kwamba Nchi zinazolingiza silaha zimetoa leseni za uingizaji nje ya nchi au idhinisho; na
- (b) kwamba, bila ya kuathiri masharti mengine ya mikataba baina ya nchi mbili, mikataba baina ya nchi nyingi au makubaliano kuhusiana na nchi zisizo na bandari, nchi zinazotumika kwa kupitishia bidhaa, kwa masharti ya chini kabisa, zimetoa taarifa ya maandishi kabla ya bidhaa kusafirishwa, kuwa hazina pingamizi kuhusiana na upitishaji huo wa bidhaa katika nchi zao;

3. Leseni ya usafirishaji nje ya nchi na ya uingizaji ndani ya nchi au uidhinishaji na nyaraka yoyote inayoambatana nayo itakuwa na taarifa kwamba, kwa masharti ya chini kabisa, itakujumuisha sehemu na tarehe ya kutolewa, tarehe ya kuisha muda wake wa kutumika, nchi inayosafirisha silaha, nchi ambayo silaha inaingizwa, nchi ya mwisho ambayo silaha zitapokelewa, maelezo na idadi ya silaha au vipuri vyake, pamoja na silaha, na iwapo kutakuwa na upitishaji wa silaha ndani ya nchi, majina ya nchi ambazo kupitia kwake bidhaa zinapitishwa. Taarifa iliyo katika leseni ya uingizaji wa silaha ndani ya nchi ni lazima itolewe mapema kwa nchi ambazo kupitia kwake silaha zinapitishwa.

4. Nchi Mwanachama inayoingiza silaha, baada ya kuwasilishwa maombi ya kufanya hivyo, itaitaarifu Nchi Mwanachama ambayo inasafirisha bidhaa nje ya nchi kuwa imepokea silaha au vipuri vyake, pamoja na risasi zilizosafirishwa.

No.2 Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi 2015 93

5. Kila Nchi Mwanachama, kupitia njia zilizokaribu yake, zitafuata masharti, kadri ambavyo itakavyohitajika ili kuhakikisha kuwa taratibu leseni au uidhinishaji ni wadhati na kwamba uhalali wa utoaji wa leseni au nyaraka za uidhinishaji zinaweza kuthibitishwa au zimethibitishwa.

6. Nchi Wanachama zinaweza kufuata taratibu za kawaida kwa ajili ya uingizaji ndani ya nchi, usafirishaji nje ya nchi na upitishaji ndani ya nchi wa silaha au vipuri vyake, pamoja na risasi kwa muda, kwa madhumuni yanayothibitika kama vile uwindaji, ulengaji shabaha kwa ajili ya michezo, tathmini, maonesho au ukarabati.

Imepitishwa na Bunge Tareh 19 Machi, .2015

THOMAS D. KASHILILAH
Katibu wa Bunge